# NJIA YA UANAFUNZI KUWA TIMOTHEO

Nicholas Jackson

# YALIYOMO

**DIBAJI** ………………………………………………………………… 3

**UAMSHO WA UANAFUNZI** ……………………………….. 7

**NIFUATE MIMI - NJIA YA UANAFUNZI** ………………… 16

**NIFUATE KAMA NINAVYOMFUATA KRISTO** ……….. 22

**KUWA TIMOTHEO - UANAFUNZI NA MAFUNZO** ….. 27

**KUWA TIMOTHEO - KUTUMWA KAMA MWANA** …… 33

# DIBAJI

Nilizaliwa Mara ya pili kwa kwa kukutana na kumpokea Yesu katika mwaka wa 2001. Maisha yangu yakageuka kwa ghafra. Mwerekeo wa maisha yangu ukageuzwa, na nikafahamu nimeitwa kuhubiri Injili. Lakini nilikuwa sina namna ya kuihubiri Injili na pia nilitakikana nikomae. Hata hivyo, nilimpenda Yesu na Neno na nikalipokea neno kila Siku.

Baada ya miaka kadha ya kujaribu kufanya kazi katika huduma za chuo, nikifanya kazi katika huduma za vijana katika ushirika wa mahali pamoja, na nikitafuta mwito wa Mungu, nikawa na shauku ya baba. Nilitaka mtu ambaye anaweza kunifundisha kumuishia Yesu. Sikuridhika na kuenda mikutano ya kanisa. Nilitamani niwe mwanafunzi. Nilitaka kile wale thenasara walikuwa na Yesu. Nilitaka kile Timotheo alikuwa na Paulo. Nilitaka baba.

Aya katika Malaki **4:5-6** ilininenea. Niliona panatakiwa urejesho wa ***"Mioyo ya baba kwa wana na mioyo ya wana kwa baba".*** Kutoka kwa aya hii moyo wangu ulianza kumlilia baba. Nilijua ndani yangu nimeitwa kama mtume na nikajua nilimhitaji baba ili anionyeshe njia ya kufanya kazi hiyo.

Katika majira hayo ya kumtafuta Mungu katika roho yangu, na katika kukutana na watu wengi na huduma njiani, niliongozwa kukutana na mtume kwa jina Paul Galligan mwisho wa katikati wa mwaka wa 2005. Mara ya kwanza nilisikia akifundisha, alifundisha ujumbe wa "Uwana", jinsi ya kufanyika wana waliokomaa wa Mungu.

Katika mkutano huo nilipatana na Mungu ambapo roho yangu ilianza kulia "Baba yangu, baba Yangu". Mara nikafikiri kuhusu **2 Wafalme 2: 1-12 w**akati Elisha alimwona Eliya akichukuliwa mbinguni na akalia kilio kile. Mungu akanena nami akasema, "ninayafanya

mambo mawili ndani yako: Ninakufanya mwana (mwana aliyekomaa) kwangu; na ninakupa Paulo (Galligan)kama baba wa kiroho".

Katikati ya mwaka 2006 nikamwambia Paul kwamba nataka kuacha kila kitu ambacho nilikuwa nikifanya, nije na niwe naye katika huduma na nifanywe mwanafunzi na nitayarishwe naye kama "Timotheo". Aliniomba niondoka na nimuone tena baada ya miezi sita nieleze kama hitaji hili lingalipo. Hii ni  ya muhimu. Ningependa uone kwamba mimi, kama mwana, ndiye nilianzisha uhusiano wa baba/mwana. Na Paul akaonyesha hekima kwa kujaribu uwazi wangu kwa kuwa ni ya muhimu kutofanya maamuzi haya kwa msingi wa musisimuko ama kwa kuongozwa na bidii ya nafsi.

Mnamo mwanzo wa 2007, niliishi na Paul kwa nyumba yake kwa majuma mawili wakati wa shule ya kuandaliwa na nikaonyesha kwamba nilikuwa na utayari wa kupeana kila kitu nilichokuwa nikifanya ili nijipeane kwa uanafunzi kikamilifu, yeye akinifundisha. Mungu alikuwa amedhibitisha ndani ya moyo wangu wakati huo. Paul alinijibu kwa njia hii, "Ye*su alikuwa na wanafunzi kwa miaka mitatu. Walikaa na yeye. Walijifunza huduma kwa kuwa Naye. Timotheo alitembea na Paulo akifanya hayo. Ukiyataka hayo basi ujipatiane kwa kuja (hapa Toowoomba) na ukae nami miaka mitatu. Hiyo itakuwa ni mafunzo yako"*. Haya ndiyo moyo wangu kwa hakika ulitamani katika Bwana na tukapatana.

Safari ya uanafunzi ilikuwa imeanza kwangu. Nilifanya kila kitu na Paul. Nilifanya kazi na yeye mashinani nikitumika katika huduma.Tuliomba pamoja kila siku.Tulijifundisha neno pamoja.Tukamega mkate pamoja. Nikaona na kujifundisha njia ya maisha ya kuwa mwanafunzi wa Yesu. Nilienda na kikundi katika Australia na kwa mataifa mengine pamoja naye. Kisha akaanza kunifundisha kufundisha na kuhudumu. Nilipoandalika, Paul akaanza kunituma kwa umisheni. Nikatumwa na hatimaye nikawekwa wakfu kufanya kazi kama mtume wa Yesu Kristo. Na hata leo "***Ninatumika naye kwa ajili ya Injili, kama mwana na baba yake"*** **Wafilipi 2:22.**

Kwa wakati huu nimejifunza mambo mengi. Nimejifunza jinsi mamlaka ya kweli huja kupitia kunyenyekea. Nilijifundisha jinsi ya kumsikia Mungu na kuongozwa na Roho wa Mungu. Nimetambua zaidi "***utajiri wake Kristo usiopimika***" **Waefeso 3:8.** Nimejifunza faida ya kujipatiana, kunyenyekea, uaminifu, utiifu, kurekebishwa, kufundishwa na utayari wa kutubu na kubadilika. Nimejifunza jinsi ya kuwajibika kibinafsi na kwa wengine. Nimejifunza jinsi ya kuwaangalia watu wa Mungu kwa moyo mweupe. Na cha muhimu zaidi, nimejifunza jinsi ya kumwona Mungu katika Neno Lake, kupokea ufunuo na kuwa na uwezo wakuwalisha watu wa Mungu kwa "***maarifa na fahamu***" **Yeremia 3:15.**

Sasa tunaweza kufika bali. Kama vile nimekuwa mwaminifu katika uwanafunzi, Mungu amefungua ufunuo na ufahamu kwangu kutoka kwa maandiko, na sasa huduma inaweza kufika maeneo kwingi, mataifa mengi. Mungu hupanua kazi Yake kupitia wana. **Mungu analitimiza neno lake kupitia Malaki 4: 5-6!**

Kijitabu hiki kimeandikwa kutusaidia sisi wote kuingia urejesho huu na uamsho. Kumekuwa na uamsho mwingi katika historia ambapo Mungu amekuwa akirejesha ukweli katika kanisa.Tuko katika nyakati ambapo Mungu anarejesha Ukristo wa kitume - ambao ni uanafunzi ukielekeza kwa wana waliokomaa.

Mungu anahitaji wana. Wana waliokomaa ambao wanatembea naye kama jinsi Yesu alitembea. Anawainua akina baba katika siku hizi ambao wana moyo wa wana. Jambo sio kuwa na wana kwa ajili yao lakini kuwainua wana wengi kutembea katika ukomavu wakiwa na Mungu kama baba yao. Paulo alimuinua Timotheo. Eliya alimuinua Elisha. Musa alimuinua Yoshua. Yesu aliwainua wale thenashara. Kuna muundo. Haina utaratibu wa idara. Haiwezi kuwa. Inaongozwa na Roho na ni kazi ya ndani ya Mungu.

Nimebarikiwa kuwa na baba katika Bwana ambaye ameniinua niwe mhuduma anayefanya kazi na mwenye mazao kama sehemu ya kikundi cha kitume cha watakatifu kilichopeanwa kutimiza agizo la

Yesu la kuwafanya wanafunzi katika mataifa yote. Mimi ni sehemu ya kazi ya kijamii. Mimi ni sehemu ya kazi ya Baba yangu.

Unaposoma kijitabu hiki, naomba kwamba Roho wa Hekima na ufunuo atakuja juu yako kuona jinsi urejesho umekata kwa moyo wa kile tunaita "kanisa" Yesu anatuita tufanye Mambo njia Yake.

Kwa neema Yake, ninahusika na ni mshirika wa Mungu akirejesha uhakika wa baba\mwana wa kanisa. Hatuhusiki na idara. Sisi ni washirika wa nyumba ya Mungu (**Waefeso 2:19)** na katika nyumba hiyo kuna watoto wachanga, vijana na akina baba **(1 Yohana 2:12-14).** Ni jamii, sio idara.

Ni wakati wa uhusiano wa kweli wa uanafunzi kwa Yesu na neno lake kurejeshwa. Ni wakati wa viongozi wa huduma kupokea moyo wa Baba na Mwana na kwa dharura kufanya wanafunzi na kukuza kizazi kingine cha wana ambao watarithi nchi, "***ahadi zote za Mungu"*** katika Kristo (**2 Wakorintho 1:20).**

Nicholas Jackson, August 2019

# UAMSHO WA UANAFUNZI

## Uamsho wa Uanafunzin

Katika siku hizi za urejesho wa kitume na marekebisho ya kanisa, kuna uamsho mkubwa unaofanyika kati ya watu wa Mungu duniani kote. Roho anasema kwa makanisa "waamke kwa uanafunzi". Ni wakati wa kizazi kuamka kwa uhitaji mkubwa wa uanafunzi wa kweli na hitaji kubwa la Yesu kufanya na kuwa na wanafunzi! Uamsho mkuu wa kizazi chetu ni uamsho wa uanafunzi.

- ***Uamsho mkuu wa kizazi chetu ni uamsho wa uanafunzi***

## Wito wa Yesu katika Injili

Yesu alikuja kuwaita wanafunzi. Yesu alikuja kuwaita watu ambao wangetamani kuwa wanafunzi, wakihitaji kuelekezwa katika njia mpya ya maisha na wakiwa na nia ya kumuiga. Yesu anataka ***"mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu"*** **Mathayo 11:29.** Wito wa kuwa mwanafunzi ni wito wa kujifunza kutoka kwa Yesu. Injili ni wito wa uanafunzi kujifunza njia za ufalme kwa kujishikilia kama kishikamanishi kwa Mfalme.

## Tubu

Wakati Yesu alianza huduma yake, Alihubiri ***"Tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia"*** **Mathayo 4:17.** Uamsho wa kila mmoja wetu unaanza na mwito wa kutubu, kutamani kubadilika. Tunatakiwa kuwa na kutamani mabadiliko katika mawazo yetu, kubadilisha njia zetu, nia zetu, ili tujifunze kuishi katika ufalme wa mbinguni.

***Uanafunzi ni kujifunza jinsi ya kuishi katika ufalme wa mbinguni tukiwa katika ulimwengu. Lazima tutamani kubadilika!***

## Wito katika uanafunzi

Baada ya kuhubiri hitaji la kutubu, Yesu akaendelea kuwaita watu wachache "***Yesu aliwaona ndugu wawili Simoni aitwae Petro, na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi, Akawaambia , Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu"*** **Mathayo 4:18-19.** Inawezekana na yaweza kuwa, ya kuwa Simoni na Andrea walitumainia wito huu. Walikuwa sehemu ya uamsho uliokuwa ukifanyika mto Yordani kupitia Yohana mbatizaji **(Yohana 1:35-42)** na Andrea alikuwa amemsikia Yohana akitangaza Yesu kuwa yule "***Mwana kondoo wa Mungu"*** **(Yohana 1:36).** Walimjua Yesu. Walijua kile ambacho Yohana alikuwa amenena kumhusu Yesu. Mioyo yao ilikuwa ikimshaukia Masihi. Mioyo yao ilikuwa tayari kumfuata Yesu. Mioyo yao ilikuwa tayari kwa uanafunzi.

## Mwaliko

Leo, kitu kinatendeka kwa watu wa Mungu ambacho kinawaandaa kwa uanafunzi. Watu wanataka kutoka kwa taratibu za kidini na katika kunaswa katika "kanisa". Kuna kiu cha kumfuata Masihi. Kuna kiu cha kuhusika katika ufalme na katika kazi ya Yesu. Kuna kutamani kwa kujua uhakika wa kumfuata Yesu kila siku kama njia ya maisha. Mwaliko ni wa ajabu! "***Nifuateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu".*** Tunatakiwa "***Tufuate"*** Yesu. Tunatakiwa kutazama jinsi anavyoishi, tukiangalia kila hatua yake, ili tuweze kujifundisha kuwavuta wengine katika misha yake.

Huu ni mwaliko wa kujifundisha kuishi. "***Njia mpya na iliyo hai"*** (**Waebrania 10:20*).*** Ni wakati Wa kuachana na kila tunachokitenda ***'Mara wakaziacha nyavu zao wakamfuata"*** **Mathayo 4:20.**

## Unaishi kwa kusudi gani?

Ni wakati wa kuchunguza tunaishi kwa kusudi gani. Msukumo wetu ni upi? Malengo yetu ni yapi? Kwa nini tuko hai? Yesu alisema ***"Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate"*** **Mathayo 16:24. Kujikana** ni kutoishi kwa agenda yetu ama mambo yanayotupendeza. ***Kuuchukua msalaba*** **ni**

***"kusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake"* (Wagalatia 5:24)** kujikana wenyewe na hali inayotupendeza. Ni kufa katika hali ya matamanio yetu binafsi. Jina ***fuata*** linamaanisha *kuwa njia Moja, kuambatana.* Yesu anataka twende safari Naye. Yesu anataka tuambatane ili tujifunze kutenda atendayo. Ili tuyatende haya, ni lazima tupatiane kila tulicho nacho.

## Kuyapoteza maisha yetu ili tuyapate ndani ya Yesu

*Uamsho wa uanafunzi* ni kupokea ufunuo kwamba kuambatana na Yesu inafaa kupoteza kila kitu kinginecho "***kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona"* Mathayo 16:25.** Maisha yanapatikana katika uanafunzi. Uzima wa milele unatabulika tunapoupoteza uhai wa nafsi zetu kwa ajili ya kumfuata Yesu! Ni nini unachoishi kwa ajili yake? Marehemu Jim Elliot, mmishonari ambaye alijitoa maisha yake katika miaka ya 1950 alipokuwa akifikia kikundi cha watu ambao walikuwa hawajafikiwa katika Merikani Kusini, aliweka msemo huu. "*Sio mjinga mtu ambaye anatoa kila ambacho hawezi kuhifadhi ili apokee ambacho hawezi kupoteza".* Yesu ndiye kila kitu ambacho kinahitajika. Hebu tufanye maamuzi kwa pamoja ***"kuyahesabu mambo yote kuwa hasara ... kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo"* Wafilipi 3:8.**

## Mungu anahitaji kila kitu

Mungu kila mara amekuwa akihitaji kuhusika katika kila eneo la maisha yetu. Hakupanga tuwe na maisha yaliogawanyika katika sehemu na maeneo tofauti. Anataka kuwa kwa kila kitu. Agizo lililo kuu kulingana na Yesu ni ***"sikiza, Ee Israeli, BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja, nawe mpende BWANA, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote" (*Kum 6:4-5, Mariko 12:29-30).**

## Amri kuu

Amri kuu inaanza na kukiri Mungu ni nani, kwamba, ***Yahweh Mungu wetu, ndiye mmoja.*** Yesu alifungua hii zaidi aliposema "***Mimi na Baba tu umoja***" **Yohana 10:30.** Yesu ndiye ufunuo wa huyu Mungu mmoja. Ni yeye Yahweh katika mwili, ***"alipoonekana ana umbo kama mwanadamu"*** **Wafilipi 2:8a.** Yeye ndiye mwanzilishi wa maisha ya uanafunzi. Yeye ni Mungu akituonyesha jinsi ya kuisha katika mwili. Tunapaswa kuwa na kukiri kwa Yesu kama Mungu mmoja wa kweli na tunatakiwa kumpenda na utu wetu wote. Hii ni kwa bidii kumpa ukuu katika maeneo yote ya nafsi zetu, uweza wetu wote na uweza wa utendaji, na kumtumikia kwa roho zetu katika Injili (**Warumi 1:9).**

## Kuishi mtindo wa Maisha

Baada ya kutuambia amri kuu kisha Mungu anatuambia kupitia Musa funguo za kufanya haya. Ni kwa kukuza mtindo wa maisha ukijizingira na njia ya maisha ya mbinguni "N***a maneno haya ... yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo, yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako"*** **Kum 6:6-9.**

- ***Ni kwa kukuza mtindo wa maisha ukijizingira na njia ya maisha ya mbinguni***

## Uzingirwe na Neno

Twapaswa kujizingirwa na Neno. Twapaswa kunena Neno. Twapaswa kupumua Neno. Twapaswa kuzungumza neno na tufundishe watoto wetu wa kiasiri na wa kiroho.. Kila nyumba inastahili kuwa mahali Yesu anaheshimiwa. Kila nyumba yapaswa kuwa mahali jamii wanakutanika kwa Neno wakijifunza kuhusu Yesu na kuelekezwa katika njia zake. Je, huwa unawafundisha watoto wako Neno la Mungu? Chochote tukitendacho tunastahili kukitazama kupitia Neno kisha tukifanye kwa Jina la Bwana wetu Yesu, kwa utukufu wa Mungu

(**Wakolosai 3:17, 1Wakorintho 10:31*).*** Huu ndio uamsho wa uanafunzi!

## Mazungumzo ya Mbinguni

***"Uraia wetu ni mbinguni"*** **Wafilipi 3:20.** Neno uraia limetafsiriwa kutoka katika KJV kama "***mazungumzo".*** Hii inazungumzia njia yetu ya maisha. Kuzungumza kwetu njia ya uzima, inastahili kuwa ya mbinguni. Kusudi ya kujizingira na neno ni "***ndipo ujitunze, usije ukamsahau YAHWEH"*** **Kum 6:12.**

## Dumu katika Neno

Wanafunzi ***"hukaa ndani ya neno langu... Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"*** **Yohana 8:31-32.** Huu ndio uamsho mkuu wa uanafunzi. Ni mabadiliko katika mtindo wa maisha. Sio sana kwenda kwa "mikutano ya kanisa". Ni maisha ya kuishi. Maisha katika Neno, kupumua Neno ili ***"neno lifanyike mwili"*** **(Yohana 1:14)** ndani yetu na watu watauona utukufu wake!

## Mtindo wa maisha wa kanisa la kwanza.

Katika **Mdo 2:42 t**unaona muundo wa mtindo wa maisha wa wanafunzi. ***"Wakawa wakidumu katika fudisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali".*** Ikiwa, kama wanafunzi, tutajipatiana katika nidhamu hii tutapata kumuhisi Yesu miongoni mwetu: uzima wa Mbinguni ukitiririka duniani.

Huu ndio mtindo wa maisha ya mbinguni:

**a)** ufikie Neno, ambalo ni ***fundisho la mitume***

**b)** uchangie katika ***ushirika*** wa upendo wa kweli pamoja na wanafunzi wengine ukidhihirisha upendo Wake kupitia ushirikiano wetu katika Kristo **(Yohana 13: 34-35).**

**c)** kufikia ushirika wa mwili na damu ya Yesu katika meza ya Bwana, ***"kuitangaza mauti ya Bwana hata ajapo"*** **1Wakorintho 11:26,** ambayo ni ***kumega mkate;***

**d)** na kufikia Bwana kwa pamoja kupitia ***maombi "kwa ajili ya watu wote, kwa wafalme, na wote wenye mamlaka"*** **(1Timotheo 2:1-2) na** kuomba ***"ufalme wake uje na mapenzi yake yatimizwe duniani kama huko mbinguni"*** **(Mathayo 6:10).**

*Huu ndio mtindo wa maisha ya wanafunzi katika uamsho! Watu wanaoonyesha njia mpya ya maisha, wakiishi katika ufalme wa mbinguni duniani!*

## Zaidi ya kuwa Mkristo mzuri

Watu wengi wamezuiliwa kwa uanafunzi. Yule Kijana tajiri mtawala alikuwa kama wakristo wengi leo wakitafuta sababu ndogo ya "kuokoka". N***itende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele?*** **Mathayo 19:16.** Yesu akamwambia huyu mtu azishike amri na yule mtu kwa moyo akajibu haya yote nimeyashika lakini akasema, ***" nimepungukiwa na nini tena?"*** **(aya 20).**

## Kuna kitu kinapungua

Kuna upungufu mkubwa katika mwili wa Masihi. Watu wengi wanajitahidi kuwa "Wakristo wazuri". Wanamuamini Yesu, wanalipa fungu la kumi na ni 'washirika wazuri wa kanisa' wakihudhuria ibada za Jumapili. Wengi pia wanaweza kufaulu katika mambo mengi tofauti. *Lakini kuna kitu kimepungua!*

## Usikose Mwaliko

Wakati kijana huyo mtawala tajiri aliuliza nimepungukiwa na nini, Yesu aliweza kumjibu kwa njia nyoofu, "***ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo unifuate"*** **Mathayo 19:21.** Yesu alitoa mwaliko wa nguvu kwa mtu huyu. Huyu mtu alikuwa mwamini "mzuri" wa Mungu. Alikuwa anatii amri lakini kuna kitu kilipungua. Yesu alimpa huyu mtu nafasi ya umilele**- *"njoo unifuate".***

## Nafasi ya uanafunzi

Yesu alimpa nafasi ya uanafunzi. Ilimaanisha kwamba alitakiwa kuyaacha maisha yake ya kawaida. Ilimaanisha awache starehe zake na usalama wa fedha, "***uza ulivyo navyo".*** Ilimaanisha hapana kuwa na uzima wake tena katika mali yake, ***"uwape maskini".*** Hii ilikuwa ni nafasi ya umilele - lakini aliipoteza! Alipoteza nafasi ya kupata maisha kamili katika ufalme wa mbinguni. Alipoteza nafasi ya utajiri wa milele wa utukufu wa Mungu,***"hazina mbinguni".*** Alikosa kupokea ufahamu wa ***"siri ya ufalme wa Mungu"*** **(Mathayo 13:11)** na "***utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu"*** **(Waefeso 1:18).** Alitupilia nafasi ya uanafunzi abaki kuwa "mkristo mwema mshiriki wa kanisa".

## Kuna dhawabu kuu

Kuna dhwabu kuu na utosherevu katika kupokea mwito wa uanafunzi. Kwa kijana tajiri mtawala aliyetupilia nafasi, kulikuwa tu na huzuni, "***Yule kijana aliposikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi"*** **(Mathayo 19:22).** Tusipopokea mwito wa uanafunzi tutakuwa na kutoridhika, huzuni na kutofurahia baraka ya kutimiza hatima na mwito wa Mungu katika maisha yetu.

## Kujua dhawabu inatusaidia kupeana kila kitu.

Lakini wakati tunatambua ukuu wa dhawabu inastahili kutusaidia kuweka kila kitu kado. "***Amin, nawaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi Mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli. Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapokea mara mia, na kuurithi uzima wa milele"*** **Mathayo 19:28-29.**

## Uanafunzi unafaa

Mtume Paul anasema ***"Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu Bwana wangu"*** **Wafilipi 3:8.** Dhawabu ya uanafunzi ni kubwa**.**

Inatuelekeza kwa urithi wetu.Tunapata kufahamu kwa kweli Yesu Masihi kwa hakika.

- ***Dhawabu ya uanafunzi ni kubwa. Inatuelekeza katika urithi wetu. Tunapata kufahamu kwa kweli Yesu Masihi kwa uhakika.***

## Mitume wako miongoni mwa watu wa Mungu.

Inaonekana kwamba kwa jumla katika "kanisa" la leo ulimwenguni bado kuna migawanyiko kati ya "viongozi na washirika", kati ya wahuduma na watu. Hii sio kitume. Huu sio uanafunzi. Wakati Paul alinena na Wathesalonike alisema, ***"ya kwamba Injili yetu haikuwafikia katika maneno tu, bali na katika nguvu... kama vile mnavyojua jinsi ziilivyokuwa tabia zetu kwenu, kwa ajili yenu. Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana..."*** **1Wathesalonike 1:5-6.**

## Mitume hupeana  mfano kwa watu wa Mungu.

Kama mitume, Paulo aliishi miongoni mwa wale aliowahudumia. Aliwaonyesha mfano wa tabia, mazungumzo na mtindo wa maisha. Aliweza pia kuwaambia kwamba ***"Walifanyika wafuasi wetu na wa Bwana".*** Neno ***wafuasi*** hapa linamaanisha *waigaji.* Wathesalonike walikuwa na uweza wa kumuiga Paulo na mtindo wa maisha wa kikundi chake. Mitume wanahitajika katika uamsho wa uanafunzi kwa sababu wanaweza kusema "***mnifuate mimi kama mimi  ninavyomfuata Kristo".*** **1 Wakorintho11:1.**

## Jifunze, pokea, sikia na uone

Wakati Paulo aliwaandikia Wafilipi aliweza kusema, ***"mambo miojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi"*** **Wafilipi 4:9.** Mitume wamepatianwa kuleta muundo huu kanisani. Kanisa katika maandiko sio idara lakini ni jamii na kikundi cha wanafunzi ambao wanajifunza maisha mapya. Mitume na washirika wote wanatakiwa kutoa mfano wa jinsi ya kumfuata Yesu.

Paulo anashiriki nasi sifa nne zinazohitajika kwa wanafunzi kukutana na Mungu wa amani kutoka **Wafilipi 4:9.**

- ***Kanisa katika maandiko sio idara, lakini ni jamii na kikundi cha wanafunzi ambao wanajifunza maisha mapya.***

**a)** ***Mambo uliojifunza* -** wanafunzi ni wale ***wanaojifunza* -** lazima tuwe na kupenda kusoma, uwe mtu anayefundishika na anayeweza kurekebishwa

**b)** ***Na kupokea* -** tunapaswa ***kupokea*** kutoka kwa mitume, na viongozi wengine wa kitume, kupokezwa na upako wa Roho, kwa kuwa nao **(Warumi 1:11, 2 Timotheo 1:6).**

**c)** ***Na kusikia* -** wanafunzi wanatakiwa kuwa ***wanaosikia* -** wakifundishwa Neno, fundisho la mitume, kikamilifu ili walipitishe kwa kizazi kingine **(2 Timotheo 2:2).**

**d)** ***Na kuyaona ndani yangu* -** wanafunzi wanatakiwa kuwa ***wanaona* -** wakitazama na kuiga mtindo wa maisha ya Kiungu na njia ya maisha ya mitume na viongozi wa kitume. (**1 Wakorintho 4:16-17, 2 Timotheo 3:10-11).**

## Ni wakati wa kurejerea kwa ukristo wa kitume

Uamsho mkuu katika kizazi chetu uko hapa. Ni wakati wa kurejerea kwa ukristo wa kitume, ambao ni uamsho wa uanafunzi. Itahitaji **kujipatiana** kukubwa. Itahitaji **utiifu.** Itahitaji **kuhesabika.** Itahitaji neema na **utume.** Mungu amerejesha huduma ya kitume kanisani Iili kuwa na kuongezeka kwa wanafunzi ambao wanajua kufuata Yesu na waishi na "***mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo"*** **(Wafilipi 1:27).**

## Ni wakati wa wanafunzi kuongezeka

Mitume wakiweko na wakifanya kazi. "***Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalemu; jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile Imani"*** **Mdo 6:7.** Kama haujajiunga tayari, ni wakati wa kujiunga na uamsho mkuu na kuingia katika himaya ya uanafunzi wa kweli. Ingia katika uamsho wa uanafunzi!

"***Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana ... jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile Imani"*** **Mdo 6:7.**

# UNIFUATE MIMI - NJIA YA UANAFUNZI

## Wito ni wa kufuata

Yesu ndiye mfano timilifu wa vile uanafunzi unafanya kazi katika ufalme wa Mungu. Wakati Yesu alianza huduma yake, aliwaita wengine "***Nifuateni mimi"*** **Mathayo 4:19.** Hakuwaita katika mfumo, taasisi, seminari ama kwa wazo la shule ya Theolojia**. Aliwaita kwa mtindo wa maisha mapya.** Aliwaita wafute mfano wake.

## "Fuata"

Neno ***"fuata"*** katika **Mathayo 4:19** linamaanisha kutembea nyuma, ama *kuja nyuma* ya mtu ama kitu. Tumeitwa tuwe nyuma ya mfalme "***Nayo itazifanya hatua zake kuwa njia"*** **Zaburi 85:13.** Ahadi yake ni kwamba tukifuata njia hii "***Nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu*"**.** Uanafunzi unatubadilisha! Tutafanyika kitu tofauti kuliko tulicho sasa.

## Walimfuata

Wakati Yesu aliwaita ndugu, Simoni Petro na Andrea, ***"Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata"*** **Mathayo 4:20.** Neno "***wakamfuata"*** hapa ni tofauti na neno katika **Mathayo 4:19.** Neno hili linamaanisha: *kuambatana, kwenda pamoja, kwenda njia moja na*... *Kuwa njia moja na mtu.* ***[***soma, utajiri wa neno katika New Spirit Filled Life Bible katika **Yohana 13:36].** Tumekaribishwa na Yesu tujiunge Naye katika njia ile anayoendea. **Tumekaribishwa kutembea Njia moja.** Uanafunzi inahusika na kuwa na muungano wa njia pamoja na Yesu na kujifunza Njia ya kutembea, Njia ya kuendea, Njia ya kwa Baba **(Yohana 14:6).** Ni mwaliko wa mtindo wa maisha ya Masihi.

## Watu wa "Njia"

Wanafunzi wa kwanza walijulikana kama watu ***"wa Njia".*** Kabla ya Sauli kujulikana kama mtume Paulo alikuwa akiwaangalia ***"watu wa Njia hii...awafunge na kuwaleta Yerusalemu"*** **Mdo 9:2.** Ingawa Sauli

"***nikawaudhi watu wa Njia hii hata kuwaua"*** **(Mdo 22:4),** alimalizia kuungama, "***kwamba kwa Njia ile ambayo waliita uzushi, ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu"*** **Mdo 24:14.**

Kuwa katika Njia hii inatuwezesha kumwabudu Mungu katika kweli. Uanafunzi, Njia ya Yesu, inatusababisha kumjua Mungu na kupata kumwabudu Yeye. Ufahamu wa Mungu hupatikana katika ***Njia!*** Yesu, yeye ni nani na mtindo wa maisha yake, ndiyo ***Njia*** ya kumjua Baba. Hakuna Njia nyingine.

***Uanafunzi, Njia ya Yesu, inatusababisha kumjua Mungu na kuweza kumwabudu Yeye!***

## Kaa katika njia

Mwanafunzi wa Yesu siku moja alimwambia, ***"Bwana, nipe ruhusa kwanza, niende nikamzike baba yangu"*** **Mathayo 8:21.** Yesu akamjibu kwa njia inayoonekana ya ukali, ***"Unifuate, waache wafu wawazike wafu wao"*** **aya 22.** Huyu mwanafunzi alichanganyikiwa atajitoa wapi kumuacha Yesu katika masharti yake ilikuwa ni kuiacha njia na Yesu. Yesu alimwambia ***Unifuate.*** Kwa maneno mengine, Yesu alimwambia akae akiunganika katika njia moja kama Yesu. Wengi hushindwa kwa sababu ya sababu tofauti tofauti. Wanapotoka kutoka kwa njia kwa sababu ya vitu muhimu za kuwapotosha.

## Kuna njia kuu

Kuna ahadi ya ajabu katika **Isaya 35:8, "*Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, Nayo itaitwa, Njia ya utakatifu...wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo".*** Tunastahili kukaa katika hii njia kuu na Yesu. Kama tukifanya maamuzi ya kukaa na tuendelee kutembea katika njia hiyo, hata ikionekana kuwa ngumu, ***hatutapotea*** na hatutaangamia kwa habari ya Imani **(1 Timotheo 1:19).**

## Achana na utajiri wa dunia

Yesu alimwambia yule kijana mtawala, ***"ukitaka kuwa mkamilijfu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina***

***mbinguni; kisha njoo unifuate"*** **Mathayo 19:21.** Yesu alimwalika kijana huyu aache kila kitu ambacho kilikuwa kinamzuia kuingia katika uzima wa kweli na ***amfuate*** Yeye.

## Tambua utajiri wa utukufu Wake

Kujiunga na Yesu katika Njia ni mwaliko kutoka kwa vifungo kuingia kwa faraja na utajiri wa dunia kwa ***"utajiri wa utukufu wa siri hii...Kristo ndani yenu; tumaini la utukufu"*** **Wakolosai 1:27.** Uanafunzi ni Njia ya kuwa na Kristo akiumbika ndani yako. Kumfuata Yesu ni Njia ya kumpata Mungu ***"akiwajaza kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu"*** **Wafilipi 4:19.** Hebu tuenende safari na Yesu tutambue "***kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake, katika utu wa ndani"*** ambayo ni ***"kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake"*** **Waefeso 3:16.**

## WITO WA UANAFUNZI

### 1. Wito wa kujifunza

Wakati Yesu anatuita tumfuate tunatakiwa kuchukua mtazamo wa mwanafunzi kama tutakuwa na mazao na ufanisi katika kuwa mwanafunzi. Yesu alisema, ***"jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu"*** **Mathayo 11:29.** Tumeitwa ***tujifunze*** kutoka kwa Yesu. Kujitia *nira yake* ni kujifunza kutembea Njia moja kama Yeye anapoubeba uzito na pia kufanya kazi nzito. Tukiwa na nia hii, uanafunzi utatuelekeza katika ***raha nafsini mwetu.***

### 2. Wito wa kutumika

Wito katika uanafunzi ni ***wito wa kutumika.*** Ni wito katika unyenyekevu na kujifunza kutumikia ambaye anakufunza. Yesu alisema **"*mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumwa hampiti bwana wake, yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake"*** **Mathayo 10:24-25a.** Wanafunzi hawatakiwi kuwa wakitafuta kuwasahihisha ambao wanawafunza, lakini,

wanatakiwa kutafuta kuwatumikia ili wawe kama wao. Kulingana na Yesu, wanafunzi watakiwa kutamani kuwa kama mwalimu wao.

## Elisha

Elisha "***alikuwa akimimina Maji juu ya mikono yake Eliya"*** **2 Wafalme 3:11.** Elisha alimtumikia Eliya na hatimaye akawa kama Eliya akipokea "***Maradufu"*** ya Roho aliyekuwa juu ya Eliya. Hii ilimaanisha alitumika kama mwana kwa baba maana **Maradufu** ulikuwa ni urithi wa mzaliwa wa kwanza (**Kumb 21:17).**

## Timotheo

Timotheo, ***"ametumika pamoja nami kwa ajili ya Injili, kama mwana na baba yake"*** **Wafilipi 2:22.** Timotheo, kupitia utumishi wake kwa yule alikuwa akimfunza, alikua katika huduma ya kitume yeye mwenyewe. Tena, utumishi wake ulikuwa wa mwana, sio mtumwa kwa bwana. Wanafunzi wameitwa kutumika katika injili **pamoja** na baba zao wa kiroho. Kupitia hayo watakuwa na **"*nia moja, atakayeiangalia hali kweli kweli"*** kwa wapendwa kama vile baba yao **(Wafilipi 2:20).**

***Wanafunzi wameitwa kutumika kwa Injili pamoja na baba zao wa kiroho.***

## 3. Wito Wa kufunzwa

Mchakato ambao wanafunzi wanakua ili wawe kama waalimu wao unaitwa "mafunzo". Katika **Luka 6:40** Yesu anasema, "***mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mutu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake".*** Neno ***kuhitimu*** inamaanisha *kupanga, weka kwa mpangilio, kuandaa, rekebisha, kukamilisha kinacho pungua , kuhakikisha utayari, kukarabati na kutayarisha. Utajiri wa neno katika* New Spirit Filled Life Bible [**Waebrania 11:3].**

## Jukumu la huduma tano

Jina hili linaunganishwa na neno linalotumika katika **Waefeso 4:11-12** ambalo linazungumza kuhusu huduma tano ambazo Yesu alipeana alipopaa "***kuandaa/kukamilisha watakatifu"***

Uanafunzi ni wito wa kuwekwa kwenye mpangilio ili kuweza kufanya kazi katika mwili wa Kristo. Ni wito wa kurekebisha, kukarabati, kuandaliwa na kukamilishwa. Inahitaji unyenyekevu katika kufundiswa ***kikamilifu.*** Tunatakiwa kukubali tunahitaji marekebisho. Tunatakiwa kumruhusu ambaye anatufundisha azungumze katika maisha yetu na wakati mwingine ashiriki mambo ambayo hatutaki kuyasikia. Uanafunzi ni wito wa kufundishwa!

## 4. Wito Wa kufinyangwa

Yesu aliwaambia hao wavuvi, "***Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu"*** **Mathayo 4:19.** Ni katika kumfuata Yesu tu ambapo tunafanyika kile ambacho anataka. Ni lazima tumruhusu Yesu awatumie wengine katika Mwili, ambao amechagua, kuzungumza Neno la Mungu katika maisha yetu ambalo litatufinyanga na kutupa umbo la kile ambacho Mungu ametuita tuwe. Uanafunzi ni njia ambayo tunaubwa.

## 5. Wito Wa kuwa na baba

Wakati Yesu alikuwa anazungumza na wanafunzi wake katika usiku ambayo alisalitiwa Alisema, ***"kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi,*** **Yohana 15:9.** Yesu aliwapenda wanafunzi wake kama baba, hata kama Baba. Kuwa na ufanisi wa kweli katika uanafunzi wale ambao wanafundisha wanatakiwa kubeba moyo wa Baba kwa wanafunzi nao wanafunzi wawapokee wanaowafundisha kama akina baba.

### Maneno ya mwisho ya Malaki

Haya ndiyo **Malaki** alitabiri yanatakiwa kutendeka kabla ya kuja kwa Bwana. ***"Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipige dunia kwa laana"*** **4:6.** Ni urejesho huu, kupitia uanafunzi, ambayo utasababisha viumbe, dunia yenyewe, ipate kukombolewa kutoka kwa laana (**Warumi 8:19-21).** Uanafunzi ni wito wa kuwa na baba, ili wana wengi waliokomaa wapate kufunuliwa na wairejeshe dunia! Lengo la

uanafunzi ni***"wana wengi katika utukufu"*** **Waebrania 2:10.** Wana wengi wakitembea katika ukomavu wakiwa na Mungu kama Baba yao, wakiudhihirisha utukufu wa Mungu duniani.

## 6. Wito wa kuwa marafiki.

Wito Wa uanafunzi ni hatimaye kuwa ***marafiki.*** Yesu mwishowe alisema kwa wanafunzi Wake,

***"Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo. Siwaiti tena watumwa; kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake, lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yale yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu"*** **Yohana 15:14-15.**

Marafiki ni wale ambao hawahitaji kuambiwa ambacho wanastahili kutenda. Wanafanya kwa wepesi kile ambacho wameamuriwa kutokana na ufahamu wa ndani wa Bwana na Baba.

### Marafiki wanajua mapenzi ya Baba yao

Watumwa wanahitaji kuelekezwa na kuamrishwa. Marafiki wana maagizo na maelekeo yameandikwa katika mioyo yao na wanajua ambacho Bwana na Baba anafikiri, na wanakitenda. Marafiki wanaaminiwa, marafiki ni waaninifu. Marafiki hawataondoka mambo yakiwa magumu. Uanafunzi hatimaye ni wito katika kuwa na urafiki na Yesu!

***Marafiki ni waaninifu, marafiki hawaondoki mambo yakiwa magumu, uanafunzi hatimaye ni wito wa kuwa na urafiki na Yesu!***

# MNIFUATE MIMI KAMA MIMI NINAVYOMFUATA KRISTO

## Lengo

Yesu hakuwaita watu waende wakasome katika vyeo vya Biblia vile. Alikuwa na uweza wa kusema ***nifuate.*** Mtume Paul pia hakuwaita watu katika chuo cha biblia rasmi. Alikuwa na uwezo wa kusema **"*Mnifuate Mimi kama Mimi ninavyomfuata Kristo*" 1 Wakorintho 11:1.** Hili ndilo lengo. Kua na mtindo wa maisha katika Kristo ambao unaweza kuwakaribisha wengine ndani yake. Tunapaswa kuwa na mtindo wa maisha katika Kristo ambao wengine wanaweza kufuata.

## Mtindo Wa maisha

Paulo alikuwa na uweza wa kuwaambia watakatifu katika **Filipi *"mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi"* 4:9.** Hiyo ni kali! Paul anasema kwamba *"ukiishi maisha ambayo uliona na ulitazama nikiishi, utakutana na Mungu wa amani"*. Ni kwa jinsi gani alijiamini kwa Haya? Kwa sababu mtindo wake wa maisha ulimvutia Mungu wa amani. Kwa sababu ya haya aliwaita Wafilipi kwa ujasiri wamfuate na wakutane na Mungu huyo kama yeye.

## Nifuate

Katika agano jipya kuna kauli sita za ni nini na ni nani tunapaswa kufuata. Neno ***kuiga*** imetafsiriwa ***fuata*** na limetoka kwa neno la Kiyunani *mimetes* ambapo tunapata neno la kingereza *mimic*. Hii ina maana ya kunakili, kuiga. Hebu tutazame yale tumeitwa kufuata

### 1. Fuata mtume

Mtume Paul aliwaandikia **Wakorintho, *"kwa kuwa ijapokuwa mna waalimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi. Maana mimi ndiye niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili. Basi nawasihi mnifuate Mimi"* 1 Wakorintho 4:15-16.** Paul, kama mtume ***aliwahimiza*** Wakorintho kumuiga na kufuata yeye.

### Mnifuate kwa kumpokea Timotheo

Wakorintho walitakiwa kuyafanya haya kwa njia gani? Jawabu iko katika aya ifuatayo, ***"kwa sababu hii nimemtuma Timotheo..."*** **Aya 17a.** Paul aliwaambia Wakorintho wamfuate katika kumpokea Timotheo

### Mwana mwaminifu katika Bwana

Hii inafanya kazi kwa njia gani? Maana Timotheo alikuwa ***"mwana mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakayewakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa"*** **aya 17b.** Paul alikuwa amemuinua mwana mwaminifu ambaye ***alimfuata*** Paulo. Kama ungempokea Timotheo na ujifunze kutoka kwake, ingekuwa unamfuata na kumuiga Paul! Huu ni uanafunzi njia ya ufalme wa Mungu. Ni mtindo wa maisha ukitolewa kwa kizazi kifuatacho. Ni kujifunza ***njia za mitume katika Kristo.*** Mungu anawainua mitume kwa wakati huu ambao wana maisha katika Kristo ambayo yanaweza kufwatwa.

***Ni mtindo wa maisha ukitolewa kwa kizazi kifuatacho.***
***Ni kujifunza njia za mitume katika Kristo.***

## 2. Fuata kikundi cha kitume

Paul anaandika katika **Wafilipi 3:17, "*Ndugu zangu, mnifuate mimi, mkawatazama wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi".*** KJV inaiweka hivi" ***iweni wafuasi pamoja nami".*** Tumeitwa kujiunga na mtindo wa maisha wa mitume na kuwatazama wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa "kikundi cha kitume". Mitume na wale wanatembea sawa katika uanafunzi pamoja. Huu ndio unastahili kuwa muundo wa kufuata wa watakatifu wengine.

### Kuwa wafuasi pamoja

Kikundi cha kitume kinapoendelea, wale wengine katika kusanyiko la Yesu pia wanapata mwaliko wa kujiunga wawe ***wafuasi (waigaji) pamoja nao.*** Tumekuwa na wandugu wengi ambao wameshuhudia uhakika huu wanapotutembelea. Wanaona kikundi cha wanafunzi ambacho kimejitolea wakichibua Injili pamoja.Tuna muundo,

mtindo wa maisha katika Kristo ambao tunatembea ndani yake. Kunatakiwa kuwa na vikundi vingi vya kitume ambavyo vinainuka leo, wakifuata pamoja katika mtindo wa maisha wa kitume ili wengine katika kanisa wapate kuiga njia ya kuishi ya kikundi cha kitume.

## 3. Fuata timu ya kitume

Barua ya kwanza ya **Wathesalonike** iliandikwa na ***"Paulo, Silwano na Timotheo"*** **1 Wathesalonike 1:1.** Kisha imeandikwa ***"Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana"*** **1 Wathesalonike 1:6.** Paulo, Silwano na Timotheo walikuwa timu ya kitume, wakifanya kazi pamoja. Kama timu ya kitume. Walikuwa muundo wa maisha katika Kristo ambao ungeigwa.

### Iga mwenendo wao

Mwenendo wao pamoja, mtindo wa maisha, umoja wao katika Kristo, bidii yao kwa ajili ya Injili ulikuwa wote ufuatwe na Wathesalonike. Wengine wanatuzungumzia pia kwa kuona uhakika huu tunapotuma timu kwa mataifa na miongoni mwa Australia. Wanaona jinsi timu inafanya kazi pamoja na wanaona muundo, mfano wa kuiga. Wanatabua uwasilishaji wa pande zote **(Waefeso 5:21)** na tabia zetu katika mahusiano pamoja katika Kristo na inakuwa muundo wa wengine kufuata.

### Tunakuwa mfano kwa wengine pia

Matokeo ya kufuata timu za kitume na Bwana ilikuwa ni, ***"hata mkawa (Wathesalonike) kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya"*** **Aya 7.** Walipoiga timu za kitume, wakawa kusanyiko ambalo lingeigwa na waumini wengine. Hii ndio lengo. Huu ndio uanafunzi katika ufalme Wa Mungu. Mtindo Wa maisha ukitolewa,

***"tuliona furaha kuwapa, si Injili ya Mungu tu, bali na roho zetu pia, kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu"*** **1 Wathesalonike 2:8.**

Tunatakiwa kuiga timu za kitume ili tuwe kielelezo cha wengine pia.

## 4. Fuata wazee

Tumehimizwa katika kitabu cha **Waebrania,** ***"Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao"*** **Waebrania 13:7.** Tunatakiwa kuiga imani ya wale wanaotuongoza. Tunatakiwa kuwapokea wale ambao Mungu ameteua katika maisha yetu kama viongozi katika kusanyiko na tuige imani yao.

### Chunguza sana mwisho wa mwenendo wao

Kama tunasumbuka kwamba hii ni kuongea sana kuwahusu kuwafuata watu basi kumbuka imeandikwa kwamba tunastahili tufanye haya ***"kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao".*** Kwa njia ingine, tazama tunda ambalo linatokea katika maisha yao. Kama ni dhahiri tunda nzuri iga imani yao. Njia ya uanafunzi inahusisha kuwapokea ambao Mungu ameteua katika maisha yetu kutuelekeza katika ***neno la Mungu.*** Njia ya Yesu ya uanafunzi haibadiliki, kama aya ifutayo inarekodi, ***"Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele"*** **Aya 8.** Tunatakiwa kuwaiga wazee na kutembea ***"kwa wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani"*** **2 Petro1:1.**

***Njia ya uanafunzi inahusisha kuwapokea wale ambao Mungu ameteua kutuelekeza katika maisha yetu katika neno la Mungu.***

## 5. Fuata makanisa ya Mungu

**Wathesalonike** walipongezwa na mitume, ***"maana ninyi, ndugu, mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi, katika Kristo Yesu"*** **1 Wathesalonike 2:14a.** Katika muktadha huu waliyaiga hayo makanisa ***"kwa kuwa mlipata mateso yale yale kwa watu wa taifa lenu wenyewe, waliyoyapata na hao kwa Wayahudi"*** **aya 14b.**

### Mhimizane mmoja na mwingine

Tunatakiwa kujifunza na kufuata jinsi kusanyiko linaendelea kukua na kukomaa katika Kristo ili tuweze kuvuta uwezo kutoka kwa

mmoja na mwingine na kukua kwa njia moja. Tunapaswa kupokea na kujifunza kutoka kwa makanisa mengine tukiwezeshwa na kuhimizwa na mmoja na mwingine. Tunatakiwa kuiga kusanyiko la kitume katika Kristo Yesu!

### 6. Hatimaye, fuata Mungu.

Kufuata mtume, kikundi cha kitume, timu ya kitume, wazee na kusanyiko (makanisa) mwishowe inaelekeza mahali. Hatimaye, njia hii ya uanafunzi katika ufalme wa Mungu inatuelekeza katika,

***"Hivyo, mfuateni Mungu, kama watoto wanaopendwa"*** **Waefeso 5:1.**

Katika muktadha wa **Waefeso,** Paulo amekuwa akiandika kuhusu kuvaa, ***"utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli"*** **Waefeso 4:24.** Lengo la uanafunzi hatimaye ni kutufanya kama Mungu, kupokea sura na mfano Wake.

### Kupokea sura Yake

Tunapaswa kufuata katika njia hizi zote ili tuweze ***"kufananishwa na mfano wa Mwana Wake"*** **Warumi 8:29.** Tunavaa utu upya***"unaofanywa upya, upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba"*** **Wakolosai 3:10.** Na ***"kama tulivyochukua sura yake yule wa udongo, kadhalika tutaichukua sura yake yeye aliye wa mbinguni"*** **1 Wakorintho15:49.** Twatakiwa kumfuata Mungu kama watoto wanaopenwa.

*Tunapojitolea tufanywe wanafunzi, tukijifunza kumfuata Yesu katika wale aliotuma kwetu, tukifuata mtindo wa maisha yao na njia katika Kristo, hatimaye tutapata kumdhihirisha Mungu ulimwenguni!*

*Mhimizwe kuendelesha mtindo wa maisha katika Kristo,
ambao unaweza kufwatwa na wengine.*

*Uanafunzi katika ufalme wa Mungu unakaa hivi:*

***Nifuate kama ninavyomfuata Kristo!***

# KUWA TIMOTHEO
## UANAFUNZI NA MAFUNZO

### Siku za urejesho

**Malaki** alitabiri habari ya siku za mwisho akasema, ***"Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao*** **(wana)*****, na mioyo ya watoto*** **(wana)** ***iwaelekee baba zao...*** **Malaki 4:5-6.** Tunaishi siku ambazo Mungu anafikisha ***"nyakati za urejesho wa mambo yote"*** katika kuandaa kuja kwake **(Mdo 3:19-21).** Ishara kuu ya kwamba tuko katika ***nyakati za urejesho*** ni urejesho wa baba na wana wa kiroho katika kutimizwa kwa unabii wa Malaki.

***Ishara kuu ya kwamba tuko katika nyakati za urejesho ni urejesho wa baba na wana wa kiroho katika kutimiza unabii wa Malaki***

### Baba na wana

Katika siku hizi Mungu anarejesha uhusiano wa mfano ulioonyeshwa na mtume Paulo na Timotheo. Uhusiano huu ulielekezwa na Yesu na wanafunzi wake, ***"Kama vile baba alivyonipenda Mimi, nami nilivyowapenda ninyi"*** **Yohana 15:9.** Kanisa sio taasisi, ni jamii, mahali ambapo akina baba wanawainua wana! Na uhusiano huu unaonyesha kabisa***"siri ya Mungu, yaani, Kristo"*** **Wakolosai 2:2.** Kiini na asili ya Mungu ni Baba kwa Mwana na Mwana kwa Baba. Ni katika Mwana ambapo tunamwona Baba. (**Yohana 14:9).**

### Injili huendelea kupitia wana

Ni kupitia "wana" kama Timotheo Injili inadaiwa, imetolewa na kuingizwa kimahusiano kwa kizazi kingine kama uhakika ulio hai, sio mfumo wa kidini uliokufa. Kuna kizazi cha akina "Timotheo" kiinuke na kusabaza usafi wa Injili kwa kizazi kinachofaulu! Wana waaminifu kama Timotheo wanaendelesha fundisho la kitume kwa kizazi kifuatacho cha wanafunzi **(2 Timotheo 2:2).**

## Mwanafunzi fulani

Wakati tunakutana na Timotheo katika **Mdo 16** Paulo anafanya kazi kama mtume na ako na Sila kwa timu pamoja. Inasema kuhusu Timotheo ***"na hapo palikuwa na mwanafunzi mmoja jina lake Timotheo"*** **Mdo.16:1.** Timotheo alikuwa ***mwanafunzi.*** Hii ni ya muhimu sana. Timotheo alifunzwa na makanisa katika Derbe na Listra. Yeye hakua tu mtu wa kwenda "kanisa" ama mhudhuriaji, lakini ***mwanafunzi.*** Alikuwa amekomaa akilelewa na mama aliyejaa imani **(2 Timotheo 1:15)** na aliyajua maandiko ambayo yaweza ***kukuhekimisha hata upate wokovu"*** **2 Timotheo 3:15.** Alikuwa na msingi katika Neno na alikuwa akimfuata Yesu.

## Mtazamo wa mwanafunzi

Hebu tuangalie kwa muhtasari mtazamo unaohitajika katika mwanafunzi, kwa maana hii inapatiana msingi wa kuwa mwana kama Timotheo.

- **Luka 9:57-58 -** uko tayari kuacha starehe? Kama Mwana wa Adamu uko tayari kukosa "***mahali pa kulaza kichwa chako***"? Wanafunzi wana utayari wa kuishi maisha yasio ya starehe.
- **Luka 9:59-60 -** uko tayari kuachana na maadili ya kitamaduni ambayo ni ya kijamii? Uko tayari ***"kuwaacha wafu wawazike wafu wao"*** na umfuate Yesu? Wanafunzi wana mtazamo wa kutii Yesu hata kama hiyo ni tofauti na maadili ya kitamaduni iliyopachikwa
- **Luka 9:61-62 -** uko na utayari wa kutokuwa na sababu za kijamii na kutokuwa na masharti yako ili uwe mwanafunzi? Uko tayari kumfuata Yesu pasina "***kutazama nyuma"*** kwa maisha uliyokuwa nayo? Wanafunzi hujitoa kwa wito wa Yesu na kujitoa kwa kazi ya mavuno ya ufalme bila kujizuia.
- **Mathayo 10:24-25 -** uko tayari kunyenyekea chini ya mwalimu na kutumika? Uko tayari kuwa kama mwalimu wako hata katika mateso, ***"ikiwa wamemwita mwenye nyumba Beelzebuli, je! Si zaidi wale walio wa nyumbani mwake?".*** Wanafunzi ni wale

wanaojifunza wakiwa na mtazamo wa unyenyekevu, wakiwa tayari kutumika kwa uaminifu.

- **Luka 14:26 -** uko utayari kumchagua Yesu juu ya mahusiano mengine yote? Wanafunzi wana utiifu kwa Yesu kama majukumu yote ya kuteketeza.
- **Luka 14:27 -** uko tayari ***"kubeba msalaba wako"*** na ufe kwa mapenzi yako na umwishie Yesu peke yake? Wanafunzi wanachukua mtazamo kwamba maisha yao yana maana tu wakati wanayatenda mapenzi ya Mungu, sio mapenzi yako.
- **Luka 14:33 -** uko tayari kuachana na mali yako na kutofungwa na mali yako? Wanafunzi wanatumia walivyo navyo kwa sababu ya ufame wa Mungu na kuchukuwa mtazamo wa "***walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika"*** **Mdo 2:44-45.**

*Hii ndio mitazamo ya mwanafunzi. Hii ndio mitazamo iliyokuwa na Timotheo na ikampa msingi wake kuwa mwana kwa mtume Paulo na kufundishwa katika huduma.*

## Timotheo alishuhudiwa mema

Katika kanisa la Listra na Ikonio Timotheo ***"alishuhudiwa vema"*** **(Mdo 16:2).** Hii inamaanisha kwamba alikuwa mwanafunzi mzuri, akionyesha mitazamo ya mwanafunzi. Inaonyesha Timotheo alikuwa ni mtu mtiifu, akinyenyekea kwa wazee na kwa mwili (**1 Petro 5:5, Waefeso 5:21).** Wakati tunatii na ***"kujifunga unyenyekevu"*** tunapokea neema kutoka kwa Mungu ya kufanya kazi kama mwanafunzi na mshiriki wa mwili.Timotheo alikuwa na uhusiano mwema na wazee na watakatifu. Alikuwa amejitolea na kuwajibika katika mwili, sio aliyekuwa akifanya mambo yake mwenyewe. Timotheo alikuwa sehemu ya mwili wote akikua mbele yao wote.

***Alikuwa amejitolea na kuwajibika katika mwili, sio aliyekuwa akifanya mambo yake mwenyewe.***

## Timotheo alikwenda katika timu

Wakati haya yote yalipomfikia Paulo ***"akamtaka huyo* (Timotheo) *afuatane naye*** **Mdo16:3.** Timotheo alikuwa amekua kama mwanafunzi miongoni mwa makanisa na sasa ulikuwa ni wakati wa mafunzo na mtume kama baba wa kiroho. Kama baba, Paulo alitambua mwito wa Timotheo katika maisha yake na alitaka utimilike. Paulo, kama baba, alikuwa na mtindo wa maisha ambao Timotheo angefuata na ajifunze nao. Timotheo alikuwa akisonga ngazi ingine kutoka kwa ***Wanafunzi hadi kwa mafunzo.***

## Nifuate mimi

Kwa kuja kwa timu, Paulo anamkaribisha Timotheo katika maisha yake katika Kristo. Hii sio ya siku zetu katika vyuo vya biblia. Hii ni katika mafunzo kazini, kuishi kama familia siku zote kila siku. Timotheo alikaribishwa ndani ya maisha ya Paulo kama vile wale wanafunzi kumi na wawili walikaribishwa ***"wapate kuwa pamoja naye*** **(Yesu)" Mariko 3:14.** Huu ndio urejesho. Baba wa kweli ambao wanaweza kusema ***"Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo"*** **1 Wakorintho 11:1.** Yesu alisema ***"Nifuateni... "*** **Mathayo 4:19.** Baba wanatakiwa kutoa mtindo wa maisha kwa wana na kuwaalika wana kuwafuata na kuiga njia zao. Timotheo alikuwa tayari kujifundisha kikamilifu kuhusu kazi ya utume. Kile ambacho Timotheo alikuwa tayari kujifunza hakiwezi kutolewa kwa chuo cha mafunzo cha Biblia. Ni ujuzi katika uhusiano na baba, kufanya kazi pamoja na baba.

## Kujifunza katika timu.

Wakati Timotheo alijiunga na Paulo na Sila katika timu alipata uzoefu wa mambo mengi ambayo hangejifunza katika darasa kwa shule tu.

- ✓ **Mdo. 16:6-10 -** Timotheo alijifundisha jinsi haswa ya kuongozwa na Roho Mtakatifu katika kuamua ni wapi ataihubiri Injili.
- ✓ **Mdo. 16: 11-15 -** Timotheo alijifunza jinsi ya kuleta jamii nzima kwa Yesu, kuwabatiza na kupanda kanisa katika nyumba.

- ✓ **Mdo. 16:16-24 -**Timotheo alitazama mgongano wa ufalme wa Mungu na ufalme wa giza na jinsi hii inaweza kuelekeza mateso na kufungwa.
- ✓ **Mdo. 16:25-34 -** Timotheo aliona jinsi ya kumsifu Mungu kwa vitendo katikati ya mateso na kuona upenyo wa Mungu na nguvu za miujiza. Aliona katika ukombozi wa Mungu kutapatikana wokovu na wanafunzi wengi kupatikana na makanisa mengi ya nyumbani kupandwa.
- ✓ **Mdo 16:35-40** - Timotheo alijifunza, kwa kumtazama Paulo, sio kwa kusukumwa huku na huko na mamlaka lakini kusimama sehemu yako na kuwa kichwa wala sio mkia katika Kristo (**Waefeso 1:20-23, 2:5-6).**

*Mambo haya yote Timotheo alijifunza katika Injili ya kweli na baba wa kiroho ambaye alikuwa akifanya kazi!*
*Unaenda na wanafunzi katika timu anapohudumu? Unawapa wanafunzi ujuzi katika uwanja? Unawainua akina "Timotheo"?*

## Maarifa kwa uzoefu

Uzoefu wangu ni kwamba unajifunza mambo mengi ukiwa katika timu. Nilijifunza mambo mengi sana nikiwa na mtume Paulo Gilligan. Nilijifunza kwa kuwa naye katika kanisa la nyumbani, na kwa kuenenda katika timu ng'ambo na katika Australia. Niliona jinsi alikabili hali fulani katika maombi na pia katika matendo. Niliona jinsi aliomba na kubabanua mambo ya kiroho, kushinda mashambulizi ya uchawi na ushawishi wa mapepo. Niliona jinsi kama mtume alitumia mamlaka juu ya wakuu na nguvu katika ulimwengu wa rohoni.

## Roho Mtakatifu analeta kumbukumbu.

Sasa, ninapoenda katika misheni, ninaona vile baba yangu anafanya nami nayafanya hayo. ***"Masikio yangu yanasikia sauti nyuma yangu, ikisema, njia ndiyo hii ifuate, mgeukapo kwenda mkono wa kullia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto..."*** **Isaya 30:21. H**aya hutendeka wakati Roho Mtakatifu ananikumbusha jinsi nilivyomwona

baba wa kiroho akifanya kazi katika hali kama hiyo. Ninapokabiliana na hali fulani, ananikumbusha Yale niliyoyaona baba wangu wa kiroho akifanya nami naweza kuyatenda hayo pia. Kama uonavyo, hii ni zaidi ya mafunzo ya Biblia peke yake.

# KUWA TIMOTHEO - KUTUMWA KAMA MWANA

## Kujifunza uvumilivu

Baada ya Paulo, Sila na Timotheo kuwa Thesalonike na Berea, Wayahudi kutoka Thesalonike waliwafuata na walitaka kila mtu amuinukie Paulo. Inasema katika **Mdo 17:14, "*mara hiyo wale ndugu wakampeleka Paulo...bali Sila na Timotheo wakasalia huko*".** Neno hili ***wakasalia*** ni sawa na neno linalotafsiriwa ***kuvumilia*** katika **Mathayo 24:13, *"Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka"*.** Neno hili linamaanisha *kungojea kwa utulivu na ujasiri, kuwa na upinzani Wa nguvu unaofanya kazi* {Word Wealth Mathew 24:13, New Spirit Filled Life Bible}. Timotheo alijifunza kuwa na nguvu na ukali katika hali ngumu. Alijifunza kutorudi chini. Paulo akamwambia baadaye,

***"Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu"***
**2 Timotheo 2:3.**

## Uzalishaji wa Tabia.

Kuwa "Timotheo" inatoa nafasi ya kuzalisha tabia ambayo inayohitajika katika kuumbika katika sura ya Kristo. Kwa kujifunza kuvumilia alijifunza kwamba "***kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo, na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini"*** **Warumi 5:4.** Paulo aliweza kusema kwa Timotheo baadaye ***"ila mwajua sifa yake"*** **Wafilipi 2:22a.**

## Tabia hutangulia karama

Watu wengi katika ulimwengu wa Kanisa hupewa vyeo kwa sababu ya karama, karama za kiroho na utu. Hata hivyo, wana kama Timotheo, wanakua katika tabia ili waweze kuendesha majuku ya kijamii ya Injili. Baba wa kweli kama mtume Paul wanahitaji zaidi kukuza tabia katika wana wao kuliko kuona tu udhihirisho wa karama. Wanatabua kwamba karama bila tabia inaweza kumharibu mtu lakini

karama juu ya msingi wa tabia zilizojaribiwa, zitafaidi kila mtu, zikiwa***"kwa kufaidiana"*** **1Wakorintho 12:7.**

***Baba wa kweli kama mtume Paulo, wanahitaji zaidi kukuza tabia katika wana wao kuliko kuona tu udhihirishoho wa karama.***

## Kupokea maagizo

Baada ya Paulo kuwaacha Timotheo na Sila kule Berea kisha inasema, ***"lakini wale waliomsidikiza Paulo wakampeleka mpaka Athene; nao wakiisha kupokea maagizo kuwapelekea Sila na Timotheo, ya kwamba wasikawie kumfuata, wakaenda zao"*** **Mdo 17:15.** Inaonekana kwamba kama baba Paulo alikuwa na haki ya kutoa maagizo kwa Sila na Timotheo. Timotheo alikuwa ni mwana mwenye utayari wa kuambiwa jinsi ya kufanya. Hakufikiria kwamba angebakia Berea na kuanzisha huduma yake bila Paulo. Wale walio wana kama Timotheo wanajifunza kwamba wao ni sehemu ya jamii na wana utayari wa kupokea maagizo, kutoka kwa baba. Timotheo alikua katika mamlaka kwa sababu ya kutii mamlaka. **Mamlaka ya kweli huachiliwa katika utiifu.**

*Mamlaka ya kweli huachiliwa katika utiifu.*

## Wana ni nguvu za baba

Wakati Paulo hatimaye alifika Korintho alikuwa peke yake, alianza kazi ya hema na ***"Akatoa hoja zake katika sinagogi kila sabato"*** **Mdo 18:4.** Hata hivyo, ***"Hata Sila na Timotheo walipotelemka kutoka Makedonia, Paulo akasongwa sana na lile neno, akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo"*** **Mdo 18:5.** Jambo lilitendeka kwa Paulo wakati wana wake walipofika! Wakati Sila na Timotheo walipofika Paulo ***akashawishiwa na Roho Mtakatifu!*** Hii ina maana akashikwa na kuelekezwa na Roho kushuhudia kwa nguvu. Wakati akina baba wana Timotheo, hii inaleta ujasiri na ushujaa kwa baba ikimwezesha kushuhudia katika hali ngumu. Soma **Zaburi 127** kuona wana ni baraka kwa akina baba, hata ***"wanaposema na adui langoni"***

## Usiharakishe mafunzo

Ninakumbuka wakati mtume Paul Galligan aliniambia kuhusu kutodhihirika katika huduma kabla ya wakati. Alinikumbusha kwamba Yohana mbatizaji ***"Alikaa majangwani hata siku ya kutokea kwake kwa Israeli"*** **Luka 1:80.** Inaonekana pia Timotheo alikuwa na Paulo mda mrefu kabla ya kuwachiliwa pekee katika huduma. Alikaa chini ya mafundisho na mafunzo. Alikuwa na Paulo katika Korintho ***"mwaka mmoja na miezi sita akifundisha kati yao neno la Mungu"*** **Mdo 18:11.**

Hii ilikuwa ni miezi mingine kumi na minane juu ya mda ambao Timotheo alikuwa na Paulo. Alikuwa ameketi chini ya mafundisho, akimtumikia baba yake. Yesu pia alijifunza kutoharakisha. Alisubiri hata alipofikisha umri wa miaka thelathini kabla ya kuingia kwenye huduma **(Luka 3:23).** Kama Timotheo kuna umuhimu wa kupoteza tamaa ya "kutaka kuwa kitu". Ngonjea wakati wa Mungu uwachiliwe katika huduma ukiwa na kuungwa mkono na kutumwa na Yesu na baba wa kiroho ambaye amemweka katika maisha yako.

## Mafunzo ya ziada

Wakati timu ilienda Efeso wakaanza ***"kuhojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano. Mambo haya yakaendelea kwa mda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia (*****Jimbo la Rumi ambayo ilikuwa jiji kuu)** ***wakalisikia neno la Bwana...."*** **Mdo 19:9-10.** Timotheo alitumia miaka mingine miwili kwa uaminifu akiwa na Paulo na akawa sehemu ya mafundisho ya shule iliyokuwa ikiendelea Efeso. Wakati huu inaonekana kana kwamba Timotheo alikuwa ameanza kutumwa kwa umisheni kwa maana kupitia shule hii, Jimbo nzima walilisikia neno pasipo Paulo kusafiri popote.

## Ujuzi wa huduma.

Ngazi hiyo ingine katika mafunzo ni kutumwa nje katika umisheni na kurudi nyumbani na kuripoti **(Mariko 6:30).** Kisha kupata mafunzo ya ziada na kupata maoni na kwenda tena. Baadaye, wakati Timotheo alikuwa akifanya kazi kama mtume, pengine katika Efeso, Paulo aliwakumbusha kwamba,

***"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha wengine"* 2 Timotheo 2:2.**

Katika misheni hizi Timotheo alikuwa akijifunza kuwa mwaminifu kwa fundisho la kitume ambalo alikuwa amepokea. Akijifunza kuwajibika na sio kujaribu kuja na fundisho lake. Wana wa kitume wanatakiwa kubaki waaminifu kwa fundisho, ***"wasifundishe elimu nyingine"* 1 Timotheo 1:3.** Tunapoaminika kwa huduma ya mwingine, Mungu atatupa yetu kwa wakati ufaao (**Luka 16:12).**

***Wana wa kitume wanatakiwa kubaki waaminifu kwa fundisho.***

## Kutumwa

Mwisho wa mda huo katika Efeso Paulo alikusudia kupitia Makedonia na Akaya na ***"akatuma watu wawili miongoni mwa wale waliomtumikia kwenda Makedonia, nao ni Timotheo na Erasto, yeye mwenyewe akakaa katika Asia kitambo"* Mdo 19:22.** Neno***"kutumwa"*** hapa ni neno la Kiyunani ***apostello.*** Hii inamaanisha kwamba Timotheo na Erasto walitumwa kiutume, kumwakilisha Paulo na Yesu katika Makedonia na Akaya**.** Hii inamaana walikuwa wakienda Korintho, Thesalonike, Berea, na Filipi sasa kwa niaba ya Paulo. Waliweza kuaminiwa kutumwa kama mitume.

## Uwe na moyo wa huduma.

Ni ya kuvutia kutambua pia Timotheo na Erasto walikuwa ndio ***waliomtumikia*** Paulo. Walimhudumia Paulo. Hii ni sawa na Elisha ambaye ***"alikuwa akimimina maji juu ya mikono yake Eliya"* 2 Wafalme 3:11.** Lakini sasa wanatumwa kama wana kuiandaa njia kwa baba yao ili afike pale. Usijifikirie wewe ni mkubwa sana huwezi kutumika. Hii sio njia ya ufalme wa Mungu. **Mamlaka ya kweli ya kiroho hutokana na utiifu na huduma.**

## Mwana mpendwa na mwaminifu katika Bwana

Paulo aliwaandikia **Wakorintho** kusema, ***"Basi nawasihi mnifuate mimi"*** **1 Wakorintho 4:16.** Watakatifu wa Korintho walikuwa wamfuate Paulo kwa njia gani wakati yeye hayuko huko mwenyewe? Jawabu iko katika aya ifuatayo, ***"kwa sababu hii nimemtuma Timotheo kwenu"*** **1Wakorintho 4:17a.** Timotheo alitumwa ili kwamba Wakorintho wamfuate Paulo! Paulo alikuwa amefaulu kutoa mtindo wa maisha yake katika Kristo kwa mwana! Kisha anasema,

***"Aliye Mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakayewakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa"*** **aya 17.**

Timotheo alikuwa amependwa na alikuwa mwaminifu. Angemwakilisha Paulo kwa uaminifu kwa Wakorintho, na kwa kufanya hayo, kumwakilisha Yesu.

## Wana huubeba moyo wa baba.

Paulo aliwaandikia **Wafilipi** kwa habari za kumtuma Timotheo, akisema, **"*maana sina mtu mwingine mwenye nia moja nami, atakayeiangalia hali yenu kweli kweli*, Wafilipi 2:20.** Wana kama Timotheo wanabeba mzigo sawa na baba. Paulo anasema kwamba wahuduma wale wengine wote ***"wanatafuta vyao wenyewe, sivyo vya Kristo Yesu"*** **aya 21.** Wengine wanatafuta huduma zao wenyewe, makanisa yao, ufalme wao. Kunatakiwa kuwa na kizazi cha akina "Timotheo" kubeba moyo wa utume katika vizazi. Kisha Paulo anasema, ***"ila mwajua sifa yake, ya kuwa ametumika pamoja nami kwa ajili ya Injili, kama mwana na baba yake"*** **aya 22.** Timotheo alikuwa katika shughuli za kijamii za Injili.

## Wana hukua katika uhusiano wao na baba.

Wakati wowote ambapo Paulo alibaki kuwa baba kwa Timotheo, Paulo alitambua kukua kwa Timotheo na kukomaa. Katika mahali

kwingine Paulo alimwita Timotheo ***"Ndugu yetu, mtumishi wa Mungu katika Injili ya Yesu Kristo"*** **1 Wathesalonike 3:2.** Pia, ***Timotheo, mtenda kazi pamoja nami"*** **Warumi 16:21.** Wana wanafanyika watenda kazi pamoja katika Injili, wandugu na wahuduma, hata, ***"watumwa"*** pamoja katika kazi **(Wafilipi 1:1).** Timotheo alikuwa ni sehemu ya timu na akifanya kazi kama mtume pamoja na Paulo katika kazi **(1 Wathesalonike 1:1, 2:6). B**aba wa kweli katika imani hawataki kuwaweka wana wao chini yao. Wanataka wakomae na kufanyika ndugu na wafanyi kazi pamoja, wakiweza kuwapata wana wao pia, wakiwa baba kwa wengine.

***Baba wa kweli katika imani hawataki kuwaweka wana wao chini yao.***

## Baba huacha urithi wa wana

Wakati Paulo alikuwa akimwandikia Timotheo, ingeonekana, kwa mara ya mwisho, aliandika kuhusu urithi ambao alimuachia. Paulo alimwambia katika **2 Timotheo 3:10-12, "*wewe umeyafuata:***

- ***Mafundisho...*** Paulo alikuwa ametoa mafundisho katika maisha ya Timotheo. Alikuwa afundishe elimu ya aliyemtuma **(Yohana 7:16-18).**
- ***Mwenendo wangu ...*** Paulo alitoa mwenendo ambao Timotheo alitambua na akifanya kazi ndani yake. Timotheo alionyesha "***njia*** za Paulo ***zilizo katika Kristo"*** kwa uaminifu (**1 Wakorintho 4:17).**
- ***Makusudi yangu...*** Makusudi ya Paulo katika Injili yaliishi ndani ya Timotheo. Timotheo alibeba mioyo ya watakatifu ***"ili wao nao waupate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele"*** **2 Timotheo 2:10.**
- ***Imani ...*** Mtindo wa maisha wa imani ilionekana ndani ya Paulo ulikuwa unaishi ndani ya Timotheo. Paulo alikumbuka***"imani uliyo nayo isiyo na unafiki"*** **2 Timotheo 1:5.**
- ***Uvumilivu...*** Paulo alionyesha uvumilivu ***"kama kielelezo"*** kwa Timotheo (**1Timotheo 1:16).**
- ***Upendo...*** Timotheo aliujua Upendo wa Kristo ambao ***"watubidisha"*** Paulo **(2 Wakorintho 5:14)**

- ***Saburi ...***Timotheo alikuwa amejifunza kutokata tamaa kwa mfano wa Paulo. Timotheo alimwona Paulo *"**akistahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule**"* **(2 Timotheo 2:10).**
- ***Adha, mateso...*** Timotheo alijiunga na haya, katika korokoro pia **(Waebrania 13:23).**
- ***Naye Bwana aliniokoa katika hayo yote...*** Timotheo alijuwa ukombozi wa Bwana akijifundisha kumtumaini Mungu ambaye anawafufua wafu (**2 Wakorintho 1:9-11).**

***Huu ndio urithi wa wana***

*Inaonekana kama "**Kristo ndani yanu, tumaini la utukufu" Wakolosai 1:27.** Paulo alimuachia Timotheo mtindo wa maisha ambao ungemfunua Kristo kwa Timotheo. Paulo hakuacha sheria za kidini lakini kwa kufaulu alitoa maisha ya Kristo katika maisha ya Mwana.*

*Sasa kama ungalimwona Timotheo, ungalimwona Paulo na ungalimwona Kristo! Huu ni urejesho unafanyika katika nyakati zetu. Baba na wana wakifunua siri ya Mungu, "**siri ya Baba na ya Kristo" (Wakolosai 2:2)** kwa mfano Wa uhusiano wao!*

*Ni wakati wa kizazi cha Timotheo kuinuka ili kwamba ulimwengu uandaliwe kwa kuja kwa Yesu Masihi!*